**TAARIFA YA WILAYA YA SERENGETI**

**TAARIFA FUPI YA WILAYA KWA MAKAMU WA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA MHESHIMIWA SAMIA SULUHU HASSAN**

**Mheshimiwa Makamu wa Rais,**
kwa niaba ya wananchi wa Wilaya ya Serengeti napenda kukukaribisha katika Wilaya yetu ya Serengeti, kwani ni mara yako ya kwanza toka uchaguliwe kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Karibu sana Serengeti na ujisikie uko nyumbani.
**Mheshimiwa Makamu wa Rais,**
Wilaya ya Serengeti ni mojawapo ya wilaya sita (6) za Mkoa wa Mara.

Wilaya ina ukubwa wa km² 10,373. Kati ya km hizo, kilometa za mraba 7,000 ni Hifadhi ya Taifa ya Serengeti (Serengeti National Park),kilometa za mraba 558.9 ni eneo la "Ikorongo Game Reserve". Kilometa za mraba 434.5 ni eneo la "Grumeti Game Reserve", na kilometa za mraba 242.3 ni eneo la wazi (open area). Eneo lililobaki la kilometa za mraba 2,137.3 sawa na asilimia 20.6 ni eneo la kilimo, ufugaji na makazi ya watu.

Kulingana na Sensa ya mwaka 2012 Wilaya ilikuwa na Wakazi 249,420 kati yao wanaume ni 121,399 na wanawake ni 128,021 Ikiwa na kaya 41,570. Ongezeko la watu kwa mwaka ni wastani wa 2.8%. Kwa Mwaka 2017 Wilaya inakadiriwa kuwa na jumla ya wakazi 294,367 Wanaume 143,275 na wanawake 151,091 na kaya 49,090.

## HALI YA ULINZI NA USALAMA :

**Mheshimiwa Makamu wa Rais,** hali ya usalama wa wananchi na mali zao imeendelea vizuri hakuna matukio makubwa ya uvunjaji wa amani. Matukio yaliyopo ni madogo madogo kama vile ugomvi unaosababisha watu kujeruhiana na matukio machache ya wizi wa mifugo na makosa ya ukatili wa kijinsia. Hata hivyo matukio hayo yamekuwa yakidhibitiwa na vyombo vya Ulinzi na Usalama kufanya hali kuwa shwari.

## HALI YA KISIASA

**Mheshimiwa Makamu wa Rais,** Wilaya ina Vyama vya siasa 6 ambavyo vinaendesha shughuli za kisiasa Wilayani, Vyama hivyo ni CCM, CHADEMA, CUF, NCCR - Mageuzi, TLP na UDP. Katika uchaguzi wa mwaka 2015 CHADEMA ilishinda kiti cha Ubunge, pamoja na viti 18 vya udiwani, kati ya 30, CCM ilishinda viti 12. Madiwani viti maalum ni 11, CCM 4, CHADEMA 7. Baada ya uchaguzi vyama hivyo vinaendesha shughuli zao kwa mshikamano na amani. Halmashauri ina jumla ya Madiwani 41 kati yao 30 ni wanaume na 11 ni wanawake. Madiwani wa kuchaguliwa ni 30 na Madiwani wa viti maalum ni 11.

## WATUMISHI

**Mheshimiwa Makamu wa Rais,** Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti ina jumla ya watumishi 2,345 ikiwa ni upungufu wa watumishi 452.

**Zoezi la Uhakiki wa watumishi wa Serikali**

**Mheshimiwa Makamu wa Rais,** Uongozi wa Wilaya umeshirikiana na Serikali kuu katika uhakiki wa watumishi wa Serikali na jumla ya watumishi 2,213 wa Halmashauri ya wilaya ya Serengeti wamehakikiwa. Kati yao watumishi 43 walibainika kuwa na vyeti vya kughushi, watumishi 11 walibainika kuwa na vyeti vyenye utata na watumishi 23 walibainika kuwa na nyaraka timilifu (Vyeti). Jumla ya watumishi 54 (wenye vyeti vya Kughushi na utata) wameondolewa katika mfumo wa malipo (Mshahara).

**SHUGHULI ZA KIUCHUMI:**

**Mheshimiwa Makamu wa Rais**, Shughuli kuu za kiuchumi zinazofanywa na wakazi wa Wilaya hii ni pamoja na kilimo na ufugaji asilimia 90%. Asilimia 10% hufanya shughuli ndogo ndogo za biashara, ufugaji nyuki na uchimbaji wa madini kutokana na uchumi unaokua katika wilaya ya Serengeti wastani wa pato la mwananchi kwa mwaka 2015/2016 ni Tshs. 1,572,899/=.

**SEKTA YA KILIMO**:

**Mheshimiwa Makamu wa Rais**, Wilaya ina eneo la hekta 255,370 linalofaa kwa kilimo, hekta zinazolimwa ni 125,587 sawa na asilimia 49. Wilaya ina wakulima wanaokadiriwa kufikia 162,123. Mazao ya chakula yanayolimwa ni mahindi, mtama, mhogo, maharage, viazi vitamu, mpunga na ulezi.

Mazao ya biashara ni pamba, alizeti, tumbaku, karanga na ufuta.75% ya wakulima Wilayani hutumia Kilimo cha wanyamakazi, na 25% wanatumia jembe la mkono na matumizi ya trekta kubwa na ndogo (powertillers).

**HALI YA CHAKULA**

**Mheshimiwa Makamu wa Rais**, Kwa mjibu wa sensa ya watu na Makazi ya mwaka 2012 Wilaya ya Serengeti inao wakazi 249,420 kwa kuzingatia ongezeko la 2.8%

Mahitaji ya chakula kwa mwaka kwa kipindi cha Julai 2016 hadi Juni 2017 ni tani 92,786**.**

Aidha, katika musimu wa 2016/2017 Wilaya ililenga kulima jumla ya hekta 108,922 katika kipindi cha vuli na masika kilichotarajia kutoa mavuno ya tani 279,571 za mazao ya chakula. Hata hivyo, jumla ya hekta 98,254 za Mazao ya chakula zimelimwa; zinazotarajia kutoa mavuno ya tani 200,655. Hivyo kulingana na matarajio hayo ni wazi kuwa Wilaya ya Serengeti inatarajia kuwa na utoshelevu wa mazao ya chakula katika musimu wa 2016/2017.

**Mheshimiwa Makamu wa Rais**, hata hivyo Uongozi wa Wilaya ya Serengeti unaishukuru Serikali Kuu kwa kututengea Tani 400 za chakula cha bei nafuu(Mahindi ya msaada kutoka wakala wa taifa wa hifadhi ya chakula) chenye lengo la kupunguza mfumuko wa bei ya chakula uliokuwa umejitokeza Wilayani. Hadi tarehe 31/05/2017 jumla ya tani 224 zimepokelewa na jumla ya tani 212 zimesambazwa katika maeneo yenye uhitaji mkubwa wa chakula.Kamati ya ulinzi na usalama imekaa na kuweka utaratibu mzuri kwa

wafanyabiashara kufikisha mahindi haya karibu na wananchi ambapo wameelekezwa kuuza Tshs 700 kwa kilo kwa maeneo ya hapa mjini na Tshs 750 kwa maeneo ya vijijini.

**SEKTA YA MIFUGO:**

**Mheshimiwa Makamu wa Rais**, idadi ya mifugo iliyopo wilayani ni ng'ombe wa asili 385,542, mbuzi 151,531, kondoo 99,035, nguruwe 1,756, Punda 326, Mbwa 22,343, kuku 223,462 na bata 432. Wilaya ina ng'ombe wa kisasa 1,724 na kuku wa kisasa 1,125.

**MCHANGO WA MIFUGO KATIKA KUONGEZA KIPATO:**

**Mheshimiwa Makamu wa Rais**, Wilaya ina jumla ya minada 15, ambayo wafugaji huitumia kuuza mifugo yao. Kwa kipindi cha kuanzia Julai 2014 hadi Desemba 2015, jumla ya Ng'ombe 46,868, Mbuzi 26,304 na Kondoo 15,656 waliuzwa. Mifugo hii iliwaingizia wafugaji jumla ya Tshs. 23,238,600,000/=. Aidha halmashauri ya Wilaya iliingiza kiasi cha Tshs. 180,000,000 na serikali kuu kupita tozo za mifugo iliingiza Tshs. 5,325,500/=.

**MIKAKATI INAYOFANYWA NA WILAYA KATIKA KUIMARISHA SEKTA YA MIFUGO:**

**Mheshimiwa Makamu wa Rais,** Wilaya imeandaa Mpango Mkakati wa miaka 3 wa uzalishaji wa mifugo kwa kufuata mnyororo wa thamani wenye lengo la kuboresha maisha ya wafugaji kama matokeo ya ongezeko la kipato kwa jamii kwa kutekeleza yafuatavyo:-

- Kuendelea kutoa mafunzo kupitia mashamba darasa ili wafugaji wafuge kwa kuona na kubadili tabia ya kuona kuwa ng'ombe wengi ni utajiri.
- Kutoa elimu kwa wafugaji ili kufuga idadi ndogo ya mifugo iliyoboreshwa kulingana na eneo.

**SEKTA YA USHIRIKA:**

**Mheshimiwa Makamu wa Rais,** Wilaya ina jumla ya vyama vya ushirika vya msingi 65 mbavyo vipo katika mchepuo ufuatao; vyama vya mazao ni 12, SACCOs 41, Mifugo 4, ukamuaji mafuta 1, mapishi na mapambo 1, utumiaji umeme wa upepo 1 na vyama vya walaji (consumers) 2. Pia kuna vikundi vya Ushirika vya zao la pamba 41.

Hadi kufikia Juni 2016, vyama vya ushirika vya msingi vilikuwa na wanachama wapatao 4107 (wanaume 2654, wanawake 1453 na wanachama wa vikundi 41). Hisa na akiba katika vyama hivi zilifikia Tshs. 851,810,000.00, mikopo iliyotolewa ilifikia Tshs. 506,186,000 mikopo iliyorejeshwa ni Tshs. 4,817,913,000, mikopo isiyorejeshwa ni Tshs. 1989,470,000.

**SEKTA YA ARDHI, MALIASILI NA MAZINGIRA**

**HIFADHI YA TAIFA YA SERENGETI :**

**Mheshimiwa Makamu wa Rais,** Hifadhi ya Serengeti ina sifa mbalimbali ikiwa na Wanyama hasa nyumbu kuwa na mzunguko wa kuhama kila mwaka kwenda Masai Mara (nchini Kenya), Maswa Game Reserve,Mamlaka ya hifadhi Ngorongoro na kurudi ndani

ya Hifadhi ya Serengeti. Pia kuna Hoteli za Kitalii 5 na Kambi za Kitalii (Tented Camps) 30 na za muda 8.

**MAPORI YA AKIBA YA WANYAMAPORI YA IKORONGO NA GRUMETI:**

**Mheshimiwa Makamu wa Rais,** Wilaya ina Mapori mawili ya Akiba ya Grumeti na Ikorongo na WMA moja ambayo hutumika kwa shughuli za uwindaji wa Kitalii kuanzia tarehe 1 Julai hadi tarehe 3 Machi kila mwaka.

**●FAIDA ZITOKANAZO NA UWINDAJI WA KITALII**

**Mheshimiwa Makamu wa Rais,**Kutokana na uwindaji huo, Halmashauri ya Wilaya hupata 25% ya mapato yatokanayo na uwindaji huo. Kwa mwaka 2011/2012 Halmashauri ilipata Tshs 50,000,000/, mwaka 2012/2013 ilipata Tshs 38,000,000=, mwaka 2013/2014 fedha haikuletwa toka Serikali kuu. Aidha, kwa mwaka 2014/2015 Halmashauri ilipokea kiasi cha Tshs 139,000,000 kama asilimia 25 ya uwindaji wa kitalii. Hata hivyo fedha hizi zinapopatikana asilimia 40 hubaki Halmashauri na 60% hupelekwa kwenye Kata kama chachu ya uhifadhi wa Wanyamapori na Mazingira.

**●CHANGAMOTO ZINAZOTOKANA NA WANYAMAPORI**

**Mheshimiwa Makamu wa Rais,**pamoja na faida kubwa inayotokana na wanyama pori hawa wanayoipata wananchi wa serengeti kuna madhara makubwa yanayowakumba wananchi hasa uvamizi wa Tembo kwenye makazi ya wananchi unaosababisha uharibifu wa mazao pamoja na vifo vya wananchi na mifugo yao ambapo tangu mwaka 2009 hadi 2016 jumla ya ekari 7557.86 za mazao zenye thamani ya Tshs 1,092,016,006 zimeharibiwa na jumla ya mifugo 409 yenye thamani ya Tshs 53,570,000 imeua na wanyamapori.Aidha, kwa mwaka 2015 na 2016 jumla ya wananchi 4 wameuawa na wanyama pori.

**HIFADHI YA MAZINGIRA :**

**Mheshimiwa Makamu wa Rais,**Wilaya ya Serengeti ina maeneo ya hifadhi ya Misitu ya Asili yenye ukubwa wa kilometa za mraba 300, Hifadhi ya Misitu ya kupandwa yenye ukubwa wa kilometa za mraba 244.5. Upandaji wa miti umekuwa ukifanyika katika ngazi ya Kaya, Vijiji, Shule za Msingi na Sekondari na asasi za Serikali na zisizo za Kiserikali.
Kuanzia mwaka 2011/2012-2016/2017 jumla ya miti 6,841,684 ambayo ni sawa na silimia 76 ya lengo imepandwa.

**NISHATI NA MADINI**:

**Mheshimiwa Makamu wa Rais,** Katika Wilaya ya Serengeti kuna aina mbalimbali za madini kama dhahabu, Madini ya Chokaa na gesi aina ya Hellium yanayopatikana katika maeneo mbalimbamli. Sekta hii bado ni changa kwa sababu wachimbaji wanatumia zana duni katika shughuli za uchimbaji. Pia kwa upande wa umeme, Serengeti inatumia umeme unazalishwa na Grid ya Taifa, aidha jumla ya vijiji 52 vimepata umeme kupitia REA, vimesimamishiwa nguzo na utandazaji wa nyaya umefanyika.

**FURSA ZA UWEKEZAJI:**

**Mheshimiwa Makamu wa Rais,** Wilaya ina maeneo mengi kwa ajili ya uwekezaji katika nyanja mbalimbali zikiwemo Kilimo na Mifugo, Utalii na Maliasili, na Madini.

**Maliasili na Utalii:**

**Mheshimiwa Makamu wa Rais,** Wilaya yetu kwa sasa ina Wawekezaji waliowekeza katika maeneo ya wazi yaliyo nje ya Hifadhi ya Taifa ya Serengeti na Mapori ya Akiba ya Grumeti na Ikorongo. Mwekezaji Grumeti Reserves amepangishwa na Serikali Kuu katika vitalu (2) vya uwindaji wa kitalii anavyolipia kila mwaka. Pia amepangishwa katika kitalu cha uwindaji cha WMA na uongozi wa WMA, Grumeti Reserve hulipa ada ya uwindaji wa Kitalii ingawa kwa sasa amefanya uwindaji kwa kiwango kidogo kwa nia ya kuhifadhi wanyamapori kwa shughuli nyingine za Kitalii na kuhifadhi baadhi ya wanyama walioko katika hatari ya kutoweka kama vile Faru weusi ambapo hivi sasa kuna Faru mweusi mmoja(1) ambaye amehifadhiwa katika eneo la Vilima vya Nyabikwabi.

**Mheshimiwa Makamu wa Rais,** Wilayani Serengeti kuna maeneo mengi yenye fursa za utalii yanayohitaji wawekezaji wa nje na ndani mfano Chemichemi ya maji moto iliyoko kijiji cha Majimoto, mapango ya aina yake yaliyoko Matare, tamaduni toka makabila tofauti yaliyoko Wilayani, Ngome za Wajerumani Fort Ikoma na maporomoko ya Nyamieri kwa ajili ya Utalii wa baiskeli.

**Eneo la WMA – IKONA:**

**Mheshimiwa Makamu wa Rais,** Eneo la WMA- Ikona linaundwa na vijiji vitano (5) vya Robanda, Park Nyigoti, Nyichoka, Makundusi na Natta Mbisso ambavyo vimetoa eneo lenye ukubwa wa km  za mraba 242.3 ambalo linatumika kwa ajili ya uhifadhi wa Wanyamapori ili vijiji husika viweze kufaidika na uhifadhi wa Wanyamapori. Wawekezaji ndani ya eneo hili ni Moivaro Investment Ltd, Grumeti Reserves Ltd,. Zara International Travel Agency, Thomson Safari, Tusks  Tours, Serengeti Simba Safaris Ltd, Grumeti Hill na Well Wealth lodges and hotels Ltd.

**SEKTA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

**Mheshimiwa Makamu wa Rais,** Wilaya imeendelea kuboresha makazi ili wananchi wamiliki maeneo yaliyopimwa kisheria na waweze kutumia hati za viwanja kwa ajili ya kupata mikopo kwenye taasisi ili kuongeza kipato. Upimaji kutokana na mgawanyo wa vijiji uliofanyika kati ya mwaka 2009 na 2014 tuna jumla ya vijiji 78 kati ya hivyo vijiji 5 vina vyeti vya kijiji, vijiji 43 vimepimwa na vinaandaliwa vyeti vya kijiji na vijiji 30 havijapimwa.Aidha, kwa mwaka 2016/2017 vijiji 6 kati ya 15 vinavyozunguka hifadhi ya Taifa ya Serengeti vimetengenezewa matumizi bora ya ardhi.

**SEKTA YA MIUNDOMBINU:**

**Mheshimiwa Makamu wa Rais,** Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti inasimamia matengenezo ya barabara zenye mtandao wa **Km 753**, kati ya barabara hizi **Km 183.40** ni

za changarawe na **Km 569.60** ni za udongo.  Kwa sasa asilimia **72** ya barabara zinazohudumiwa na Halmashauri ya Wilaya zinapitika kwa mwaka mzima.
Kwa mwaka wa fedha 2016/20167Halmashauri ya wilaya ya Serengeti imeidhinishiwa kiasi cha Tshs. **1,736,600,000** kwa ajili ya matengenezo mbalimbali ya barabara. Kazi zilizopangwa kufanyika ni ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami nyepesi km. **2**, matengenezo ya barabara km 282.51 (Matengenezo ya kawaida 210.5 km, matengenezo ya sehemu korofi 42.1 km, matengenezo ya muda maalum 26.91km na ujenzi wa makalvati 30). Kati ya **Tshs. 1,736,600,000**/= zilizoidhinishwa, **Tshs. 700,000,000/=** ni kwa ajili ya matengenezo ya barabara ya lami nyepesi Mugumu mjini 2km ambapo kazi hiyo imetangazwa na wakandarasi wanaendelea kuchukua vitabu vya zabuni.
Matengenezo mengine ya km 282.51 utekelezaji wake uko 45%

**SEKTA YA ELIMU:**

**Mheshimiwa Makamu wa Rais** Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti inazo Shule za Msingi 115 (111 za Serikali na 4 za binafsi). Shule za Sekondari zipo 26 kati ya hizo 22 ni za Serikali na nne (4) ni za Mashirika ya dini na Binafsi, ambazo ni Issenye Sekondari, Nyabihore Sekondari, Twibhoke na Serengeti Nuru Sekondari.

**ELIMU YA MSINGI**

**Mheshimiwa Makamu wa Rais,** Wilaya ya Serengeti ina jumla ya Shule za Msingi 111 za Serikali zenye jumla ya wanafunzi 84,682 (Wav 43,934 na Was 40,748). Aidha, wilaya ina jumla ya walimu 1,157. Idadi hii haitoshelezi mahitaji kwani uwiano uliopo kati ya mwalimu na wanafunzi ni 1:60 ikilinganishwa na uwiano wa kitaifa wa1:40. Mahitaji halisi ya walimu ni 2,101 hivyo kuna upungufu wa walimu 944

**Uandikishaji wa darasa la I (2017):**

**Mheshimiwa Makamu wa Rais,** Mwaka huu, 2017,  wanafunzi walioandikishwa darasa la I wenye umri wa miaka 6 - 10 jumla ni 17,952 kati yao wavulana 9,375 na wasichana 8,577. Hii ni sawa na 133%  ya lengo lililotarajiwa kuandikishwa la watoto 13,504.

**Hali ya ufaulu Elimu ya msingi - 2017**

**Mheshimiwa Makamu wa Rais,** Kiwango cha ufaulu ni 79% ambapo kimepanda kwa asilimia 13.9 mwaka 2016 ikilinganishwa na mwaka  2015 ambapo ufaulu ulikuwa asimilia 65.  Wanafunzi wote 4,131 waliofaulu mtihani wamechaguliwa kuendelea na Elimu ya Sekondari sawa na asilimia 100.

**Utekelezaji wa agizo la Rais juu ya Utengenezaji wa Madawati**

**Mheshimiwa Makamu wa Rais,** uongozi wa wilaya ya Serengeti uliitikia wito wa Mh Rais juu utengenezaji wa madawati kwaajili ya wanafunzi wa shule za msingi na sekondari. Hadi kufikia mwisho  wa mwaka 2016, kulikuwa na jumla ya madawati 26,455 ambapo mahitaji yalikuwa dawati 22,641 na kufanya wilaya kuwa na ziada ya madwati 3,814. Hata hivyo kutokana na ongezeko kubwa la Uandikishaji wa wanafunzi wa darasa

la kwanza kwa mwaka 2017 lililosababishwa na sera ya elimu bure wilaya imekuwa na upungufu wa madawati 1,717.

**Mheshimiwa Makamu wa Rais,** kutokana na upungufu huo wilaya imejiwekea mikakati ya kuhakikisha upungufu huu unaondolewa hasa kwa wanafunzi walioandikishwa. Mikakati hiyo ni pamoja na kuingiza katika mipango na bajeti ya Halmashauri ambapo kwa mwaka wa fedha 2017/18 jumla ya Tshs 73,500,000 zimetengwa kupitia mapato ya vyanzo vya ndani na kuhimiza jamii kuchangia nguvu zao kupitia vikundi vya vijana ili tatizo la uhaba wa madawati liishe kabisa.

**MIUNDOMBINU YA SHULE**

Mheshimiwa Makamu wa Rais,hadi kufikia juni 2016 kulikuwa na jumla ya vyumba vya madarasa 795,nyumba za walimu 554,matundu ya vyoo 1,085.na ofsi za walimu 115,kwa jitihada zilizofanywa na uongozi wa wilaya kwa kushirikiana na wadau mbalimbali hadi kufikia tarehe 31 mei 2017 vyumba vya madarasa vimeongezeka hadi kufikia 839,nyumba za walimu 565,matundu ya vyoo 1,141na ofsi za walimu 147.

**ELIMU YA SEKONDARI:**

**Mheshimiwa Makamu wa Rais,** Halmashauri ya wilaya ya Serengeti ina jumla ya shule 26 za sekondari, kati ya hizo 22 ni shule za serikali , na 4 za Mashirika binafsi. Shule hizo zote zina jumla ya wanafunzi 10,630, (wav 6,304 na was 4,325). Aidha, shule hizi zina jumla ya walimu 451. Hata hivyo, wilaya ina mahitaji ya walimu wa Sayansi na Hisabati 119

**MIUNDOMBINU YA SHULE**

Mheshimiwa Makamu wa Rais,katika sekta ya elimu ya sekondari hadi kufikia juni 2016 kulikuwa na jumla ya vyumba vya madarasa 275,nyumba za walimu 116,matundu ya vyoo 442 na maabara 51,kwa jitihada zilizofanywa na uongozi wa wilaya kwa kushirikiana na wadau mbalimbali hadi kufikia 31 mei ,2017 vyumba vya madarasa vimeongezeka hadi kufikia 299,nyumba za walimu 137,matundu ya vyoo 462 na Maabara 52.

**Kuacha Shule (Drop out) kwa shule za sekondari za Serikali**

**Mheshimiwa Makamu wa Rais,** Hali ya mdondoko katika Shule za sekondari imekuwa ikijitokeza ambapo kati ya Januari hadi mei 2017 ilibainika kuwa jumla ya wanafunzi 6 wameripotiwa kuacha shule kwa sababu ya ujauzito.Aidha taarifa zao zimeshatolewa kwenye vyombo vya dola na hatua za kisheria zimechukuliwa dhidi yao.

**Uandikishaji Kidato cha Kwanza, 2017**

**Mheshimiwa Makamu wa Rais,** katika Mwaka 2017 jumla ya wanafunzi 4138 walichaguliwa kujiunga kidato cha kwanza 2017 (Was 1907 na Wav 2231). Hadi kufikia Mei 2017 jumla ya wanafunzi 3775( Was 1750 na Wav 2025) sawa na asilimia 99

walikuwa wamesharipoti shuleni. Juhudi zinaendelea kufanyika na waratibu Elimu kata, maafisa watendaji na wazazi pia kuendelea kufuatilia wanafunzi ambao hawajaripoti.

**HALI YA UFAULU KATIKA MITIHANI YA KITAIFA**

**Mheshimiwa Makamu wa Rais,** Hali ya ufaulu katika mitihani ya kitaifa imekuwa na maendeleo chanya kwa matokeo ya kidato cha II na IV kwa mwaka 2016, ukilinganisha na hali ya ufaulu kwa vidato hivyo mwaka 2015. Wakati wanafunzi waliopata daraja la I-III mwaka 2015 ilikuwa ni 22%, kwa mwaka 2016 asilimia ya ufaulu katika madaraja hayo imepanda na kufikia 28% ya wanafunzi wote waliofanya mitihani.

**SEKTA YA AFYA:**

**Mheshimiwa Makamu wa Rais,** Wilaya ya Serengeti ina vituo vya kutolea huduma ya tiba 54 ikiwemo Hospitali teule ya Wilaya ya Nyerere DDH inayomilikiwa na Kanisa la Menonite Tanzania. Kati ya hivyo 7 ni vituo vya Afya na 46 ni Zahanati. (kwa mchanganuo ufuatao vituo 36 vinamilikiwa na Serikali, 4 za watu binafsi, 2 vinamilikiwa na madhehebu ya dini na 4 za Taasisi za Serikali za TANAPA na Magereza). Aidha, Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti ina jumla ya watumishi wa kada za Afya wapatao 459 (47.9%) ukilinganisha na watumishi wanaohitajika 959 (100%) na hivyo kuna upungufu wa watumishi 500 sawa na asilimia 52.1%.Aidha,hali ya upatikanaji wa dawa muhimu ni 72%.

**HALI YA MAAMBUKIZI YA VVU NA UKIMWI:**

**Mheshimiwa Makamu wa Rais,** Wilaya ya Serengeti imeendelea kupambana na kasi ya ya maambukizi ya VVU/UKIMWI. Katika kipindi cha Januari hadi Desemba, 2015 kiwango cha maambukizi kilikuwa 3.2% hadi kufikia Machi, 2017 kiwango cha maambukizi kimeshuka kwa 0.2% na kuwa 3%. Wilaya imeendelea na shughuli za unasihi na upimaji katika vituo vyetu na Hospitali ya Wilaya (Nyerere DDH).

**Mfuko wa Afya ya Jamii (C.H.F) :**

**Mheshimiwa Makamu wa Rais,** Kwa mwaka 2016/2017 hamasa imetolewa katika Jamii Wilayani ili Wananchi waweze kujiunga na Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF), hadi kufikia machi 2017 jumla ya kaya 10,992 sawa na 26.4% ya kaya zote 41,570 zilikuwa zimejiunga na mfuko huu.

**SEKTA YA MAJI:**

**HALI YA HUDUMA YA MAJI WILAYANI:**

**Mheshimiwa Makamu wa Rais,** Mahitaji ya maji Kiwilaya ni Mita za ujazo 42,438 kwa siku na upatikanaji wa maji ni Mita za ujazo 24,275 kwa siku sawa na asilimia 57.2 ya mahitaji. Kaya zinazopata huduma maji ndani ya Mita 400 ni 16,628 kati ya kaya 41,570 sawa na asilimia 40 ya kaya zote. Wilaya ina vyanzo maji 597 (visima virefu 72, vifupi 160, miradi ya maji mtiririko 20, miradi ya kusukuma maji kwa mashine 35, matanki ya

kuvuna maji ya mvua 136, malambo 52, vyanzo vya asili vilivyoboreshwa 120 na mabwawa 2).

**MRADI WA MAJI CHINI YA PROGRAM YA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA VIJIJINI:**

**Mheshimiwa Makamu wa Rais,** kwa kutambua umuhimu wa Maji, Wilaya ya Serengeti ina miradi 11 inayosimamiwa na Halmashauri inayotarajiwa kuhudumia wananchi katika vijiji 12. Miradi 9 ujenzi wake umekamilika; miradi miwili (Kebanchabancha na Nyamitita/Kenyana) imechelewa kukamilika kutokana na ukosefu wa fedha.

**Mheshimiwa Makamu wa Rais,** Hata hivyo, kwa sasa taratibu za kuendelea na ukamilishaji wa miradi hii zinaendelea. Changamoto kuu tunayokabiliana nayo katika miradi hii iliyokwisha kamilika ni wananchi kutochangia huduma hivyo kusababisha Kamati za maji kushindwa kutoa huduma kwa kukosa fedha za mafuta ya kuendeshea mitambo. Elimu imeendelea kutolea kwa Jumuiya za watumia maji pamoja na wananchi wote kwa ujumla.

**HUDUMA YA MAJI KATIKA MAMLAKA YA MDOGO WA MUGUMU:**

**Mheshimiwa Makamu wa Rais,** Mahitaji ya maji katika maeneo ya mamlaka ya mji mdogo wa Mugumu ni mita za ujazo 2,532 kwa siku, ambapo utoaji huduma ni mita za ujazo 1,519 sawa na asilimia 60 ya mahitaji.

**Mheshimiwa Makamu wa Rais,** pamoja na upatikanaji huo wa maji katika mamlaka ya mji mdogo wa mugumu, bado kuna changamoto ya ubora wa maji yanayosambazwa. Hata hivyo katika kutatua changamoto hii tuna mradi wa Ujenzi wa Chujio "Treatment Plant" ambapo hadi sasa kazi ya ujenzi wa chujio inaendelea kwa kumtumia mkandarasi **M/S PET COORPERATION LTD** chini ya usimamizi wa mamlaka ya maji Musoma**(MUWASA)** .Mkandarasi huyu anatarajiwa kukamilisha na kukabidhi mradi huu tarehe 30 juni 2017 na wakazi wa Mugumu watapata maji safi na salama.

Aidha, changamoto nyingine ni gharama kubwa za kiundeshaji ukilinganisha na maduhuli yanayokusanywa, uwezo mdogo wa tanki kulinganisha na mahitaji ya sasa pamoja na kuchakaa kwa miundombinu ya mtandao wa mabomba.

**SEKTA YA MAENDELEO YA JAMII:**

**Mheshimiwa Makamu wa Rais**, Halmashauri ya Wilaya Serengeti imeendelea kutoa mikopo kwa makundi ya Vijana na Wanawake kwa mujibu wa maelekezo ya Serikali. Katika mwaka wa fedha 2014/2015 hadi Machi 2016/2017 Halmashauri ya wilaya imetoa mikopo kwa vikundi 67 vya wanawake yenye thamani ya Tshs. 118,000,000/= na vikundi 42 vya vijana vimepewa mikopo yenye jumla ya Tshs. 159,500,000/=, kati ya hizo Tshs. 107,000,000/= ni mapato ya ndani na Tshs. 52,500,000/= ni mkopo kutoka Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo.

**Vita dhidi ya Ukeketaji**

**Mheshimiwa Makamu wa Rais**, uongozi wa wilaya kwa kushirikiana na jamii pamoja na wadau wa maendeleo tumeendelea na kampeni ya kutokomeza Ukeketaji kwa wasichana.

Aidha, uongozi wa Wilaya unatekeleza kampeni hii kwa kushirikiana na Shirika la Amref Health Africa na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu.

**Mheshimiwa Makamu wa Rais**, kampeni hii inayotekelezwa inajulikana kama ***Tokomeza Ukeketaji*** katika Wilaya ya Serengeti; ambayo kwa kiasi kikubwa imesaidia kupunguza wimbi la ukeketaji toka wasichana 14,122 waliokeketwa mwaka 2014 hadi kufikia wasichana 5,621 waliokeketwa kwa mwaka 2016.

**MPANGO WA KUNUSURU KAYA MASIKINI (TASAF III)**

**Mheshimiwa Makamu wa Rais,** Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti ni miongoni mwa Wilaya **168** nchini zinazotekeleza Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini (TASAF III) unaolenga kutoa ruzuku kwa kaya masikini ili kujiongezea kipato na kujenga rasilimali watu hususan watoto. Utekelezaji wa Mpango wa TASAF III Wilayani Serengeti ulianza rasmi mwezi Julai, 2014 ambapo ulihusisha **Vijiji 57** vilivyofanikiwa kuingia katika mpango.

**Mheshimiwa Makamu wa Rais,** jumla ya Kaya **3,666** ziliandikishwa katika Mpango Kunusuru Kaya Masikini na tayari Kaya zinazonufaika ni **3,480** kutokana na uondoaji wa kaya zilizokosa sifa. Aidha, mpaka sasa malipo kwa Walengwa yamefanyika kwa awamu nane (11). Hadi kufikia Machi, 2017 jumla **Tshs. 1,643,603,250** zimepokelewa na kiasi cha **Tshs. 1,445,904,000** kimelipwa kwa walengwa (kaya Maskini) na kiasi cha **Tshs 37,00,000** kimerejeshwa TASAF makao makuu kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo vifo, kuhama na kukosa sifa.Kiasi kilichobaki ni fedha ya uendeshaji waofisi na ufuatiliaji ngazi ya wilaya na vijiji.

**MAPATO YA HALMASHAURI YA WILAYA YA SERENGETI:**.

**Mheshimiwa Makamu wa Rais,** Makusanyo ya mapato ya ndani ya Halmashauri ya wilaya ya Serengeti yamepanda kutoka Shilingi 1,222,527,825.51 kwa mwaka 2012/13 na kufikia shilingi 3,298,258,500.00 kwa mwaka 2015/2016. Hii inatokana na kuongezeka kwa mapato yatokanayo na ushuru wa zao la Tumbaku na uwindaji wa kitalii.

**Mheshimiwa Makamu wa Rais,** uongozi wa halmashauri ya wilaya katika kuhakiksha kuwa inaziba mianya ya upotevu wa mapato **ya ndani;** katika mwaka wa fedha 2016/2017 vyanzo vyote vya mapato vinakusanywa kwa kutumia njia za kielekroniki. Lengo ni kuboresha na kuongeza ukusanyaji wa mapato kwa kiasi kikubwa.

**Mheshimiwa Makamu wa Rais,** kutokana na kutumia mfumo huo wa kiektroniki katika ukusanyaji wa mapato mafanikio yameonekana katika minada na masoko ambapo awali kwa mwezi yalikuwa na wastani wa Tshs. 20,839,000/= pasipo kutumia mashine na baada ya matumizi ya mashine za kielekroniki mapato yameongezeka na kufikia wastani wa Tshs. 32,854,000/= kwa mwezi.Hadi kufikia Aprili 2017,makusanyo ya mapato ya ndani kwa vyanzo vyote ni 75%.

**MIKAKATI YA UBORESHAJI YA MAPATO YA HALMASHAURI:**

**Mheshimiwa Makamu wa Rais,** uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya ili kuendelea kuimarisha na kuongeza ukusanyaji mapato imejiwekea mikakati ya kuibua vyanzo vipya vya mapato kwa kuanzisha maeneo mapya ya masoko wa minada. Pia Kufuatilia chanzo cha ushuru wa vitanda kilichofutwa na Serikali Kuu kirudishwe, Halmshauri ianze kukusanya.

**MAFANIKIO**

**Mheshimiwa Makamu wa Rais,** uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti umeendelea na usimamizi wa fedha na miradi na kufanikiwa kupata hati safi mfululizo kwa muda wa miaka 9.

**HALI YA RUSHWA KWA KIPINDI CHA 2012 - 2017:**

**Mheshimiwa Makamu wa Rais,** Kwa kipindi husika Halmashauri imeshirikiana na TAKUKURU na kufanikiwa katika maeneo yafuatayo:-

- Kuongeza uelewa wa wananchi juu ya makosa ya rushwa kupitia program mbalimbali za Elimu kwa Umma.
- Ongezeko la idadi ya wananchi wnaotoa taarifa za Rushwa kwa kufikia Ofisi za TAKUKURU au kuwaona Maofisa wa TAKUKURU.
- TAKUKURU imeweka utaratibu wa kushirikiana na Idara/Ofisi zingine za Serikali katika kuibua kero za wananchi na kuzitafutia ufumbuzi kwa lengo la kuongeza uwajibikaji miongoni mwa Watumishi wa Serikali.

**Mheshimiwa Makamu wa Rais,** Kwa kipindi cha mwaka 2012 hadi Machi, 2017 jumla ya wananchi **19,876** walipewa elimu ya rushwa kwa njia za Semina, Mikutano ya Hadhara, Mijadala ya wazi na kupitia midahalo.

**MIPANGO MAALUM YA WILAYA**

**Ujenzi uwanja wa ndege:**

**Mheshimiwa Makamu wa Rais,** Uwanja wa ndege unatarajiwa kujengwa katika eneo la Kijiji cha Burunga na utakuwa na Jumla ya mita za urefu 4,000 na upana wa mita 800. Uwanja huo utamilikiwa na kuendeshwa kwa ubia kati ya Halmashauri ya Wilaya na Wabia Mbalimbali akiwemo Gurumeti Fund/Reserve. Kibali cha ujenzi kutoka Serikalini kimeshatolewa na Tathmini ya athari za mazingira imeshafanywa, na cheti cha tathmini ya mazingira kutoka NEMC kilitolewa tarehe 23.10.2014.

**Ujenzi wa Barabara ya lami:**
**Mheshimiwa Makamu wa Rais,** Wilaya ya Serengeti ni miongoni mwa Wilaya zilizo kwenye mpango wa kujengewa barabara ya lami inayoanzia Makutano- Natta-Mugumu-Tabora B-Loliondo hadi Mto wa Mbu mkoani Arusha. Hadi sasa kazi ya upembuzi yakinifu ilishafanyika. Ili kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa Mradi huo Kamati ya Mikoa ya Arusha na Mara imeundwa na Viongozi wa Mikoa hiyo. Katika awamu ya I barabara hiyo imeanza kujengwa km 50 kutoka Makutano hadi Sanzate.

**Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya:**
**Mheshimiwa Makamu wa Rais,** Halmashauri imeanza kujenga sehemu ya Hospitali. Kwa kuanzia imeanzia ujenzi wa Jengo la wagonjwa wa nje (OPD) ambalo kwa sasa baadhi ya majengo yamepauliwa, ujenzi wa mradi huu (OPD) ulianza tangu mwaka 2009. Pamoja na kuanza na jengo la wagonjwa wa nje, jengo la upasuaji limekamilika kwa ufadhili wa benki ya Afrika (AfDB). Kwa jengo la OPD majengo ya TB/UKIMWI, Afya ya Mama na mtoto, kibanda cha mlinzi na eneo la kusubiria yameezekwa. Fedha zinazohitajika ili kukamilisha jengo la OPD ni Tshs 1,478,859,298 na Wilaya kwa mwaka huu wa fedha imeomba Tshs 1,000,000,000 kwa wafadhili mbali mbali ili kuendeleza ujenzi ambazo hadi sasa hazijapatikana.

**Mpango wa upimaji na uuzaji wa viwanja katika mji wa Mugumu:**
**Mheshimiwa Makamu wa Rais,** Halmashauri iko katika mpango wa kutekeleza mradi wa upimaji na uuzaji wa viwanja katika mji wa Mugumu kwa kutumia upimaji shirikishi na vyanzo vya ndani.Hadi Machi 2017 jumla ya viwanja vilivyopimwa ni 1,866 na vinatarajiwa kupimwa viwanja vingine 1,650 kata ya stendi kuu mtaa wa Bomani.

**Mpango wa ujenzi wa Chuo Kikuu Kitivo cha Maliasili na Utalii:**
**Mheshimiwa Makamu wa Rais,** Kupitia mpango wa Serikali wa kuongeza idadi ya wananchi wanaopata elimu ya juu na pia kusogeza karibu na wananchi huduma za kijamii, Serikali inatarajia kujenga chuo kikuu Kitivo cha Maliasili na Utalii katika eneo la Kisangura.

**UTEKELEZAJI WA MAAGIZO YA VIONGOZI WA KITAIFA**

- **AGIZO LA MH.RAIS LA KUFANYA USAFI KILA JUMAMOSI YA MWISHO WA MWEZI**

**Mheshimiwa Makamu wa Rais,**
Wananchi wa Wilaya ya Serengeti wamekuwa watii katika kutekeleza agizo hili.Kila ijumaa ya mwisho wa mwezi wananchi hutangaziwa kushiriki zoezi la usafi na kutojihusisha na shughuli zozote zile kwa siku ya jumamosi hadi watakapotoka kwenye usafi ambapo zoezi humalizika mnamo saa Nne asubuhi.

- **AGIZO LA MH.MAKAMU WA RAIS LA KUFANYA MAZOEZI KILA JUMAMOSI YA PILI YA KILA MWEZI**

  **Mheshimiwa Makamu wa Rais,**

  Wananchi wa Wilaya ya Serengeti wameitikia vizuri agizo lako la kufanya mazoezi kila Jumamosi ya pili ya kila mwezi ili kuepukana na magonjwa yasiyoambukizwa. Kila Jumamosi ya pili ya kila mwezi wananchi wamekuwa wakijitolea kwa wingi kushiriki mazoezi wakiongozwa na Kamati ya ULinzi na Usalama.

  **Naomba kuwasilisha.**

Nurdin H.Babu
MKUU WA WILAYA
**SERENGETI**